

11. Na Katika Maneno Yake (A.S)

Kwa mwanawe Muhammad ibnul-Hanafiyya alipokuwa akimpa bendera siku ya Jamal:

“Milima huenda ikaondoka na ikatoweka (mahali pake) wewe usiondoke! Uma meno yako. 1 Mwazime Mungu fuvu lako la kichwa chako. Imarisha nyayo zako ardhini, mtazame adui wa mbali, fumba macho yako. 2 (Yaani usiogope adui kwa kujali wingi wao na kutishika), jua kuwa ushindi ni kutoka mwa Mwenyezi Mungu swt.

-
1. Kauli yake: Uma meno yako, yasemekana mwenye kuuma meno yake mshale hauathiri ubongo wake, kwa sababu mifupa ya kichwa hukomaa na kuwa migumu. Na kauli yake: Air’Ilaha jum jumataka maana yake litumie hilo katika utii wa Mungu.
 2. Tupa macho yako; yaani, zizunguke harakati zao zote, na yafumbie macho yale yanayokutisha kutokana nao, yaani lisikutishe la kutisha bali lifumbie macho.
-